THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

015/1 **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 1**
(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

Muda: Saa 2 ***Jumatatu, 17 Oktoba 2011 mchana***

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **yote.**
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 7 zenye maandishi.

Scanned by CamScanner

SEHEMU A (Alama 10)
SUNNAH NA HADITH

1. Chagua jibu sahihi katika maswali (i) – (x) kisha uandike herufi yake katika kijitabu chako cha kujibia.

(i) Katika sheria ya Kiislamu, Sunnah inafahamika kama
A maelekezo ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa waumini.
B maelekezo ya Mtume (s.a.w) kwa waumini juu ya maisha ya dini
C matendo ya msingi aliyoyafanya au aliyoyaridhia yafanywe
D matendo bora ya Mtume, maswahaba, Tabiin na Tabi Tabiin
E tabia na mwenendo wa Mtume (s.a.w) ambao ni sehemu ya utume wake.

(ii) *"Na huzungumzi (Muhammad) kwa matamanio ya nafsi yake isipokuwa anayoyazungumza ni Wahyi uliofunuliwa kwake." (53:3-4).* Kwa mujibu wa aya hii
A Waislamu kufuata Sunnah ni jambo la lazima
B kila alilolifanya Mtume limo ndani ya Qur'an
C Mtume hakujaaliwa kuwa na matamanio ya nafsi
D mazungumzo yote ya Mtume yalilenga Qur'an
E hakuna tofauti baina ya Qur'an na hadithi.

(iii) Sababu iliyofanya uandishi wa hadithi kipindi cha Mtume uwe mdogo sana ni
A maswahaba walizoea kuandika Qur'an tu
B maswahaba wengi hawakujua kuandika
C maswahaba walikuwa na uwezo wa kuzihifadhi
D Mtume mwenyewe alikuwa hai
E Mtume aliwakataza maswahaba wasiandike.

(iv) Kazi kubwa ya pekee ya uandishi wa hadithi wakati wa ukhalifa ni
A Al-muwatta
B Al qatadaya
C Isnad Ibn Hambal
D Bukhar
E Juzuu ya Ibn Abbas.

(v) Katika elimu ya hadithi, Isnad ni
A riwaya ya hadithi
B aina ya hadithi
C wapokezi wa hadithi
D aina ya Sunnah
E maudhui ya hadithi.

(vi) Imam Malik bin Anas ni mwandishi wa hadithi aliyeinukia katika kipindi cha
A Mtume (s.a.w)
B Maswahaba
C Tabii Tabiina
D Makhalifa
E Tabiin.

Scanned by CamScanner

(vii) Kigezo kitakachoifanya Matin ya hadithi ihesabike kuwa sahihi ni
A iwe imeandikwa wakati wa Mtume (s.a.w)
B isiwe na maelezo mengi
C isipingane na Qur'an
D iwe inaeleza masuala ya kiibada
E iwe inatafsiri aya ya Qur'an.

(viii) Hadith Mutawatir ni hadithi
A iliyosimuliwa na watu zaidi ya watatu
B iliyo na sifa zote za hadithi sahihi
C ambayo Isnad yake imemfikia Mtume (s.a.w)
D inayoanza na Mtume (s.a.w) kasema
E yenye Matin na Isnad kamili.

(ix) Katika elimu ya hadithi maneno "Rawahu shaikan" humaanisha
A Abubakar na Umar
B Bukhar na Muslim
C Malik na Shafii
D Tirmidh na An-Nasai
E Hambal na Abu Daud.

(x) Jozi ipi inawakilisha tanzu ya hadithi za Mtume (s.a.w) kwa mizani ya usahihi?
A Sahihi na Ahad
B Qudussiyyi na Nabawiyyi
C Hassan na maudhuu
D Mutawatir na Ahad
E Ahad na maudhuu.

Scanned by CamScanner

SEHEMU B (Alama 15)
QUR'AN

2. Chagua kutoka **orodha B** kifungu cha maneno kinachowiana na kifungu cha maneno kutoka **orodha A**. Vifungu kutoka orodha B vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

ORODHA A	ORODHA B
(i) Soma kwa jina la Mola wako aliyeumba. (96:1).	A Madai ya makafiri dhidi ya Qur'an.
(ii) Au ndio wanasema (hivi) kuwa hii (Qur'an) ameitunga (yeye mwenyewe Muhammad)? Bali wao hawaamini lolote. (52:33).	B Wahyi wa kwanza kwa Mtume (s.a.w).
(iii) Tuongoze katika njia iliyonyooka. (1:6).	
(iv) ..., inayasadikisha yaliyo mbele yake, na ni maelezo ya Vitabu (vilivyopita). (10:37).	C Uislamu ndio mfumo kamili wa maisha.
(v) ... "(Hayo anayosimulia) ni ndoto zilizovurugika ... Basi atuletee muujiza kama walivyotumwa (Mitume) wa kwanza. (21:5).	D Qur'an haina shaka kuwa imetoka kwa Allah (s.w).
(vi) "Mbona hutuletei (hao) Malaika (wa kutuangamiza) ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli?" (15:7).	E Sababu zitakazopelekea watu kwenda motoni.
(vii) "Au utuangushie mbingu vipande vipande kama ulivyodai, au utuletee Mwenyezi Mungu na Malaika uso kwa uso." (17:92).	
(viii) Kumekughafilisheni kutafuta wingi (wa mali na jaha na watoto na kujifakhirisha kwa hayo). Hata mumeingia makaburini. (102:1-2).	
(ix) Ambao wanapuuza (maamrisho ya) Sala zao. (107:5).	
(x) "Basi nawalete Hadithi kama hizi; ikiwa wanasema kweli (kuwa hii Qur'an kaitunga Nabii Muhammad)." (52:34).	
(xi) "Qur'an ni aya za shetani", ameandika Salman Rushdie.	
(xii) Na akasema: "Hayakuwa haya (aliyokuja nayo Muhammad) ila ni uchawi ulionukuliwa (kwa wachawi wakubwa kabisa wa zamani)." (74:24).	
(xiii) Alikunja (Mtume) paji akageuza uso kwa sababu alimjia kipofu. Na nini kilichokujulisha (ya kuwa huyo Sahaba pofu hahitaji mawaidha mapya)? Labda yeye atatakasika (kwa kusikia mawaidha mapya)." (80:1-3).	
(xiv) Na (Mwenyezi Mungu) akamfundisha (Nabii) Adam majina ya vitu vyote. (2:31).	
(xv) Haya ni katika yale aliyokufunulia Mola wako katika hikima (Zake). (17:39).	

Scanned by CamScanner

SEHEMU C (Alama 15)
TAWHIID

Panga vipengele vya (a), (b) na (c) katika mtiririko wenye kuleta mantiki. Andika herufi na namba tu zinazohusika katika kijitabu chako cha kujibia.

(a) Katika Qur'an (7:158), Mwenyezi Mungu amesema:
- (i) (Mungu) ambaye anao ufalme wa mbingu na ardhi, hapana aabudiwaye (kwa haki) ila yeye;
- (ii) Na mfuateni yeye ili mpate kuongoka.
- (iii) Yeye ndiye ahuishaye na ndiye afishaye.
- (iv) Sema (Ewe Nabii Muhammad): Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote;
- (v) Basi mwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake aliye Nabii Ummy (asiyejua kusoma wala kuandika), ambaye humwamini Mwenyezi Mungu na maneno yake.

(b) Mtazamo wa Dini katika Uislamu umebainishwa vyema katika Qur'an suratul Kafirun (109:1-6) kama ifuatavyo:
- (i) Wala nyinyi hamuabudu ninayemuabudu.
- (ii) Wala nyinyi hamtaabudu ninayemuabudu.
- (iii) Nyinyi mna dini yenu nami nina Dini yangu.
- (iv) Wala sitaabudu mnachoabudu
- (v) Sema: Enyi makafiri siabudu mnachoabudu,

(c) Kwa mujibu wa Qur'an maisha ya akhera ni mchakato kama ifuatavyo:
- (i) Maisha ya Barzakh
- (ii) Kufufuliwa
- (iii) Kuhesabiwa
- (iv) Kufikwa na mauti
- (v) Maisha ya peponi au motoni

SEHEMU D (Alama 30)
FIQH

4. **Jibu kwa ufupi kwa kujaza nafasi zilizo wazi katika swali la (a) – (o). Andika neno au maneno yanayokoseana tu katika kijitabu chako cha kujibia.**

(a) Mambo anayoyafanya Muislamu katika kutekeleza swala ni (i) kumsifu na kumtukuza Mwenyezi Mungu (ii) _____ (iii) _____ na (iv) kutekeleza vitendo vya swala.

(b) Sharti za Swala ni pamoja na (i) kuchunga wakati (ii) kuelekea Qibla (iii) _____ na (iv) _____.

(c) Talaka ya (i) _____ na (ii) _____ ni aina za talaka katika jamii za Kijahilia.

(d) Maiti ya Muislamu ambaye hakufa shahidi ni faradhi (i) kuoshwa, (ii) _____ (iii) _____ na (iv) kuzikwa.

(e) Kipindi kilichoanzia karne ya pili Hijiria, kilishuhudia watu wengi waliozamia fani ya fiqh na kutoa fat-wa za ki-fiqh lakini ni fafanuzi za wanazuoni wanne tu ambazo hadi

Scanned by CamScanner

leo zilipata hadhi na umaarufu mkubwa. Fafanuzi hizo ni za: (i) Abu Hanifa IbnThabit (ii) _____ (iii) Muhammad Ibn Idris al-Shafii na (iv) _____.

(f) Haki za wazazi ni pamoja na (i) _____ na (ii) _____.

(g) Zakat ni sehemu ya (i) _____ ya tajiri anayoitoa kwa kutekeleza amri ya Allah (s.w) Mali hii sharti iwe imepindukia mwaka au baada ya mavuno na iwe imefikia (ii) _____.

(h) Mambo yanayobatilisha funga ikiwa yamefanywa kwa kusahau na mfungaji hana lawama mbele ya Allah (s.w) na swaumu yake inaswihi ni (i) _____ na (ii) _____.

(i) Usiku wenye cheo ndani ya mwezi wa Ramadhani ambapo ubora wake ni sawa na (i) _____ unaitwa (ii) _____.

(j) Hija imefaradhishwa kwa Waislamu wenye uwezo wa (i) _____ na (ii) _____.

(k) Vazi rasmi la Hija kwa wanaume wanalovaa wakati wa kuhirimia Hija au Umra huitwa (i) _____ na huvaliwa katika vituo maalum viitwavyo (ii) _____.

(l) Tawafu zipo za aina tatu ambazo ni (i) _____ (ii) Tawaful-Ifadha na (iii) _____.

(m) Kwa mujibu wa hadithi ya Mtume, mwanamke huolewa kwa (i) utajiri wake (ii) hadhi yake (iii) uzuri wake na (iv) _____ lakini katika kuchagua Mchumba Mtume amehimiza kuzingatia zaidi kigezo cha (v) _____.

(n) Katika kufunga ndoa ya Kiislamu, watu wanaoweza kuwa walii (muozeshaji) katika daraja la kwanza na la pili ni (i) _____ na (ii) _____.

(o) Katika sheria ya mirathi ya Kiislamu, usia ni ule usiozidi (i) _____ ya mali ya marehemu na uwiano wa mgawanyo wa fungu la watoto kwa mtoto wa kike akiwa pamoja na kaka yake ni (ii) _____.

SEHEMU E (Alama 30)
TAREKH

5. Chagua **neno** au **kifungu cha maneno** (i) – (xxx) ili ukamilishe kauli (a) – (o) kwa usahihi. Maneno au vifungu vya maneno vinaweza kutumika zaidi ya mara moja.

(i) Uvumilivu
(ii) Khalifa
(iii) Uhud
(iv) Majini
(v) Zakat
(vi) Al-Sadiq
(vii) Umoja
(viii) Lut
(ix) Uislamu
(x) Subira
(xi) Mtume (s.a.w)
(xii) Nabii Adam
(xiii) Al-Amini
(xiv) Mkataba
(xv) Jordan
(xvi) Jizya
(xvii) Omar
(xviii) Yatrib
(xix) Hudaibiya
(xx) Kulinda
(xxi) Daudi
(xxii) Uthman
(xxiii) Kumpwekesha Allah (s.w)
(xxiv) Kuandika mkataba wa Madinah
(xxv) Ka'abah
(xxvi) Ukweli
(xxvii) Badr
(xxviii) Uaminifu
(xxix) Ibilisi
(xxx) Musa

Scanned by CamScanner

Adui aliye dhahiri kwa binadamu ni _____ ambaye alikuwa miongoni mwa _____.

(b) Tarekh ya Kiislamu inaanza kwa kuumbwa _____ wa Allah (s.w) hapa duniani.

(c) _____ ni alama ya kihistoria iliyoko Makka inayothibitisha ukongwe wa _____.

(d) Mambo yanayoonesha kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) hakuathiriwa na mazingira yake ni _____ na _____.

(e) Wawakilishi wa Ibrahim (r.a) katika vituo vya harakati zake ni pamoja na _____ katika mji wa _____.

(f) Mtume (s.a.w) alipokwenda Mi'raji alioneshwa msikiti Aqsa kuwa ni alama ya Mwenyezi Mungu inayomhusisha _____ na _____.

(g) Mkataba wa kwanza wa Aqabah ulikuwa kati ya _____ na wageni kumi na mbili wa _____.

(h) _____ ilikuwa ni vita vya kulipiza kisasi kwa Waislamu baada ya Maquraysh kushindwa vibaya katika vita vya _____.

(i) Mtume (s.a.w) alipoota ndoto kuwa anahiji ilipelekea kutokea kwa _____ wa _____.

(j) Khalifa akiwa mrithi wa Mtume (s.a.w) kazi yake ya msingi ni _____, kukuza na kusimamisha _____.

(k) Mambo makubwa yanayodhihirisha kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa kiongozi mweledi wa Dola ni _____ na kuweka mahusiano na jirani kwa _____.

(l) Makhalifa wanne walioongoza serikali ya Kiislamu kwa nyakati tofauti alianza Abubakar (r.a) akafuatiwa na _____, _____ na wa mwisho ni Ali (r.a).

(m) _____ na _____ ni baadhi ya vyanzo vya mapato ya Dola ya Kiislamu wakati wa Mtume (s.a.w).

(n) Miongoni mwa majina ya heshima aliyoitwa Muhammad (s.a.w) wakati wa ujana wake ni _____ na _____.

(o) Waislamu wa mwanzo wa Makka walipata mafunzo ya _____ na _____ yaliyosaidia kusimamisha Dola ya Kiislamu Madinah.

Scanned by CamScanner